

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKIOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI**

SHULE YA SEKONDARI LITIPU

S.L.P 328

LINDI

/12/2020

Kumb Na. S5321/LTPSS/VOI. 1/2021

MZAZI/MLEZI WA,.....

YAH: FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Litipu kwa mwaka wa masomo 2021. Hivyo mwanao anatakiwa kuripoti Shulenii tarehe 11/01/2021 saa 1:30 asubuhi na mwisho wa kuripoti ni tarehe 29/1/2021 na mwanao/ mwanafunzi asiporipoti Shulenii Mzazi / Mlezi atachukuliwa hatua za kisheria.

**Mambo muhimu ya kuzingatia na kuyatekeza kabla ya mwanao kuripoti  
Shulenii.**

**1. AFYA**

Mwanafunzi apimwe afya yake katika hospitali ya serikali na kujaziwa fomu iliyombatanishwa na barua hii. Vipimo vifanywe dhahiri na sio vya kubuni

**2.MAVAZI**

A. SARE ZA WASICHANA

I). SKETI 2: Kitambaa Cha kijani ya jeshi Kizito, ziwe ndefu zenyé marinda zinazovuka magotini hadi kwenye vifundo vya miguuni zisizobana na za heshima.

II) MASHATI 2: Ya rangi nyeupe ya tetroni yenye mikono mifupi na yasiyobana kwa wasiovaa hijabu

III) HIJABU 2: Kitambaa chake tetroni nzito nyeupe siyo Mpira na ifunike mikono na nusu Kanzu ifike kwenye viganja na zisizobana kwa wanao vaa hijabu

IV) VIATU jozi 2: Vyeusi vya ngozi na vyenye kamba vyenye visigino vifupi

V) SOKSI jozi 2: Nyeupe tu na ndefu.

NB. Hijabu ivaliwe kwa wasichana wanaovaa nusu Kanzu tu.

## B. SARE ZA WAVULANA.

- I). SURUALI MBILI (2): Za rangi ya kijani ya jeshi kizito, iwe ndefu na chini iwe na upana stahiki, yenyen Linda mbili na yenyen turn up
- II). MASHATI MAWILI (2): Rangi nyeupe ya tetroni yenyen mikono mifupi na yasiyobana yasiwe mafupi
- III). MKANDA: Mweusi wa ngozi wa kuvalia SURUALI
- IV) VIATU Joz 2: Vyeusi vya ngozi vyenye kamba vyenye visigino vifupi
- V) SOKSI Joz 2: ndefu nyeupe

## 3. A:- MAAGIZO YA VIFAA NA SAMANI

Kila mwanafunzi anatakiwa aje na VIFAA vifuatavyo;-

- I) Spring file1. Kwa ajili ya kutunzia taarifa zake za mitiha
- II) Kamusi ( Dictionary)
- III) Seti ya Hisabati (mkebe)
- IV) Fagio la Chelewa.
- V) TSH.2000 ya vipimo vya mimba(kwa mwanafunzi wa kike)

## B:-VIFAA ANAVYOTAKIWA KUWA NAVYO

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na VIFAA vifuatavyo pindi vinapohitajika Shuleni viletwe:

- I)Panga au fyekeo
- II)Jembe kubwa
- III)Awe na VIFAA vya michezo :- raba, bukta, fulana( jezi) na trakisuti kwa wasichana

## KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE KWA MUJIBU WA SHERIA NCHINI

Shule ya sekondari Litipu ni shule ya serikali inayoendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu nchini. Ukiwa mwanafunzi katika shule hii unatakiwa kuzingatia na kuheshimu;-

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

A.Kila mwanafunzi anawajibika na kuwa na heshima na adabu kuanzia nyumbani, Shuleni na mitaani

B.Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya Kati yake na mwanafunzi mwenzake, kwa mwalimu na watu wengine

C.Ni lazima kuonyesha moyo wa kushirikiana, huruma, upole na kusaidiana katika shughuli mbalimbali pamoja na kazi

D.Mwanafunzi anatakiwa kusimamia na kusalimia na kupokea mzigo wa mwalimu au MTU yoyote anayemzidi umri

E.Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu bila idhini toka kwa Mkuu wa shule

F.Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya Mambo yafuatayo:-

I)kuvuta sigara/ bangi ama kutumia madawa ya kulevyia

II)kuvaa mavazi yasiyo na heshima Kama kulegeza SURUALI na Nguo za kubana

III) kupiga kelele darasani

IV)kufuga kucha ndefu, kuwa na nywele zisizokubalika na chafu ,kuvaa mapambo ,kujipaka Rangi katika kucha na midomo( hasa wasichana)

V) kunyoa nywele katika mitindo isiyokubalika

VI) kucheleta kufika Shulen,kutofanya kazi katika eneo alilopangiwa na kutohudhuria vipindi darasani

VII)kutochomea shati na kuva suruali bila mkanda( wavulana)

VIII)Ni marufuku kuva viatu vya wazi ( sandals)

IX) Ni wajibu wa Mzazi / Mlezi kutoa taarifa endapo mwanafunzi amepata matatizo ya kiafya au kifamilia

X)kuingia kumbi za starehe, vigodoro,kuangalia video usiku, vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni.

XI)Utoro wa rejareja ni kosa lisilovumilika na taarifa yoyote ya zarura apewe mwalimu wa darasa au mbadala wake na si vinginevyo.

#### **G. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

I. Wizi

II.Uasherati,ubakaji,ushoga,ulawiti, na usagaji

III.Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia,biashara ya madawa yoyote ya kulevyia

IV.Ujauzito

V.kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, mtumishi au mwalimu

VI.Makosa ya jinai (kuua,kuiba)

VII.Kuharibu kwa makusudi mali ya shule/umma(ya watu wengine)

VIII.Kuo au kuolewa,kupata mimba au kusababisha mimba ndani nan je ya shule

IX.Kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba

X.Kugoma,kuchochea,kuongoza na kuvuruga amani na usalama wa watu

XI.Kukataa adhabu kwa makusudi

XII.Utoro wa muda mrefu

XIII.Kutumia au kumiliki simu

XIV.Kudharau bendera ya Taifa,picha za viongozi wa Taifa, nembo ya Taifa,wimbo wa Taifa na fedha za Taifa

XV.Kujiachisha shule mwenyewe.

H.Ni kosa kutoelewa sheria za shule kwa mwanafunzi

*KARIBU SANA LITIPU SECONDARI*

.....  
HASHIM B. HUSSEIN  
MKUU WA SHULE

## HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI

SHULE YA SEKONDARI LITIPU  
S.L.P 328  
LINDI  
/12/2020

KUMB.NA.LTP/SS/FI/MF  
MGANGAA MFAWIDHI.....

YAH; MWANAFUNZI .....

Amechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari mnolela mwezi januari 2021.

Kiutaratibu kabla ya kukubaliwa kuingia katika shule hii kuendelea na masomo ni lazima apimwe afya kwanza ili itusaidie kutambua afya yake.

Tafadhali nijazie sehemu inayohusika hapa chini baada ya kumpima mwanafunzi.

Asante kwa ushirikiano

.....  
HASHIM B. HUSSEIN  
MKUU WA SHULE

Tafadhali onesha mwanafunzi amewahi au ana magonjwa yafuatayo kwa kuweka alama (V) sehemu inayohusika .

- |                                         |           |             |
|-----------------------------------------|-----------|-------------|
| 1.Kifafa (opilepsy )                    | Ndio..... | Hapana..... |
| 2.Moyo (heart disease)                  | Ndio..... | Hapana..... |
| 3.Magonjwa ya akili (mental case)       | Ndio..... | Hapana..... |
| 4.Ukosefu wa damu (anemia siclecell)    | Ndio..... | Hapana..... |
| 5.Kifua kikuu (T.B)                     | Ndio..... | Hapana..... |
| 6. Pumu (Asthmatic case )               | Ndio..... | Hapana..... |
| 7.Kisukari                              | Ndio..... | Hapana..... |
| 8.Kichocho (bilharzias)                 | Ndio..... | Hapana..... |
| 9. Malaria sugu (chronic malaria )      | Ndio..... | Hapana..... |
| 10. Magonjwa ya zinaa(vernadal disease) | Ndio..... | Hapana..... |
| 11.Ujauzito                             | Ndio..... | Hapana..... |
| 12.Je? anadosari yoyote ya kiafya       | Ndio..... | Hapana..... |

JINA LA MGANGA MFAWIDHI.....

SAHIHI.....

TAREHE.....

MUHURI.....